



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MAKAMU WA RAIS



BARAZA LA TAIFA LA USIMAMIZI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA

(NEMC)

**KUFUTA USAJILI WA MIRADI ILIYOSAJILIWA KWA NJIA YA NAKALA**

**NGUMU KWAAJILI YA MCHAKATO WA TATHMINI YA ATHATI KWA**

**MAZINGIRA (EIA) NA UKAGUZI WA MAZINGIRA (EA)**

1. Kanuni ya 41A ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi) zilizofanyiwa maboresho mwaka 2018 kinaelekeza kuwa "Uhalali wa nyaraka za miradi zilizowasilishwa Baraza kwaajili ya kupata Cheti cha Mazingira utakuwa ni miaka miwili na baada ya muda huo kuisha, Baraza linaweza kufuta usajili wa maombi hayo". Kanuni imelipa Baraza mamlaka hayo ya kufuta miradi ambayo imekaa kipindi cha zaidi ya miaka miwili bila kumaliza mchakato wa EIA/EA.
2. Baraza linawataarifu wawekezaji wote ambao walisajili miradi yao kwaajili ya mchato wa EIA/EA na hawakukamilisha mchakato huo ndani ya muda uliotajwa kuwa miradi hiyo imefutiwa usajili kuanzia tarehe ya tangazo hili. Kwahiylo Baraza halitapokea nyaraka zozote zinazohusiana na uendelezaji/ukamilishaji wa maombi ya miradi hiyo ambayo orodha yake imeanishwa katika tangazo hili.
3. Hata hivyo mwekezaji anaweza kusajili upya mradi wake na kuanza mchakato wa EIA/EA kuitia mfumo wa usajili wa miradi kielektroniki [eia.nemc.or.tz](mailto:eia.nemc.or.tz).

**Limetolewa na:** Eng. Dkt. Samuel G. Mafwenga

**MKURUGENZI MKUU**